

Wingi lugha darasani

na timu ya utafiti ya
'Kuwaleta ndani walio nje'

Pointi za mazungumzo

- Je ni kwa namna gani kukosekana kwa muunganiko baina ya sera ya lugha na uhalisia wa wingi lugha kunaathiri uzoefu wa wanafunzi katika kujifunza darasani kwako?
- Ukirejelea makala, ni mbinu gani unaweza kutekeleza au umeshuhudia ambazo zinajumuisha kwa ufanisi lugha mbalimbali za wanafunzi katika mazingira ya kujifunza?
- Kwa njia zipi sera za lugha moja zinakwamisha usawa wa kielimu na ushirikishwaji, hasa kwa wanafunzi kutoka jamii zenye wingi lugha?
- Kwa kuzingatia changamoto zinazowakabili walimu katika madarasa yenye wingi lugha, ni fursa gani za maendeleo ya kitaaluma au mifumo ya usaidizi ambazo unaziona kuwa za manufaa zaidi?
- Ni kwa namna gani walimu wanaweza kushughulikia mvutano kati ya kufuata sera rasmi za lugha na kutambua wingi wa lugha ulipo miongoni mwa wanafunzi wao?
- Kwa mtazamo wako, sera za lugha zina nafasi gani katika kuendelea au kutoa changamoto kwa urithi wa kikoloni katika elimu?
- Ni kwa namna gani unaweza kuendana na nyenzo zilizopo za mtaala au maandalio ya somo ili kuendana vyema na wanafunzi wenye wingi lugha?
- Je, ni ipi baadhi ya mikakati ya kiutendaji ambayo walimu wanaweza kutumia ili kutengeneza mazingira ya darasani ambapo wanafunzi watajisi kuwezesha kutumia hazina kamili ya lugha zao?
- Ukirejelea uzoefu wako mwenyewe, ni kwa namna gani vikwazo vya lugha vinaathiri ushiriki wa wanafunzi, ushirikiano, na mafanikio kimasomo katika darasa lako?
- Ni hatua gani wadau wa elimu wanaweza kuchukua kutetea mabadiliko ya sera yanayohimiza wingi lugha na kusaidia mahitaji ya wanafunzi ya kutumia lugha zaidi ya moja katika taasisi za elimu?

Shughuli

Kulingana na timu ya utafiti, walimu wanapaswa kuona lugha zote wanazojua wao na wanafunzi wao kama nyenzo muhimu za kujifunzia, badala ya vikwazo. Katika mradi wa utafiti 'Kuleta nje ndani', waligundua kuwa walimu mara nyingi hueleza shauku ya uhitaji wa mafunzo mahususi zaidi ili kuendesha kwa ufanisi madarasa ya lugha tofauti tofauti. Kwa kuongezea, mapendekezo kutoka kwa utafiti wao yanasisitiza umuhimu wa kuwapa walimu ujuzi na usaidizi unaohitajika kufundisha katika mazingira ya lugha tofauti tofauti, pamoja na kuunda mazingira ya darasani ambayo yanasheherekea uwepo wa lugha tofauti tofauti na kutowaadhibu wanafunzi kwa kutumia lugha zao. Kama mwalimu, ni muhimu kurejelea kwenye uzoefu wako mwenyewe kuhusiana na lugha na kuzingatia jinsi unavyoweza kusaidia vyema wanafunzi wenye lugha tofauti tofauti katika madarasa yako.

Zingatia maswali yafuatayo na utengeneze ramani ya mawazo au uchanganuzi wa SWOT (Strengths, Weaknesses, Opportunities and Threats; nguvu, udhaifu, fursa na vitisho) ili kukusanya majibu yako:

- Uzoefu wako mwenyewe na lugha ni upi, kibinafsi na kitaaluma? Je, uzoefu huu umeundaje mbinu yako ya kufundisha wanafunzi wenye lugha tofauti tofauti?
- Ukirejelea uzoefu wako darasani, ni msaada gani unahisi unahitaji ili kushughulikia masuala ya lugha na kusaidia wanafunzi wanaozungumza lugha tofauti tofauti kwa ufanisi?
- Iwapo ulikuwa unahudhuria kipindi cha mafunzo kinacholenga matumizi ya lugha tofauti tofauti darasani, ni maswali gani ungeuliza ili kuongeza uelewa wako na ujuzi?
- Ni lugha zipi ambazo wanafunzi wako wanazizungumza, na ni jinsi gani lugha hizi zinaweza kuonekana kama nyenzo muhimu za kujifunzia? Je ni kwa namna gani unaweza kusherehekea na kujumuisha lugha hizi darasani kwako?
- Kwa kuzingatia mapendekezo kutoka kwa mradi wa utafiti, ni kwa namna gani unaweza kuunda mazingira ya darasa ambayo yanatia moyo badala ya kuwaadhibu wanafunzi kwa kutumia lugha zao?
- Ni kwa namna gani unaweza kutumia maonyesho ya darasa katika kukuza lugha tofauti tofauti na kusherehekea historia ya lugha tofauti tofauti za wanafunzi wako?
- Ukirejelea maarifa ya wanafunzi wako kuhusu lugha, ni shughuli gani za kujifunza ungeweza kubuni ili kuboresha ujuzi wao wa lugha tofauti tofauti na kuboresha uzoefu wao wa kujifunza?
- Je, unajua ni lugha zipi ambazo wanafunzi katika darasa lako wanazijua? Kama sivyo, je, unaweza kufikiria shughuli inavyoweza kukusaidia kuelewa vizuri zaidi kuhusu mkusanyiko wao wa lugha?

Nyenzo zaidi

Tembelea tovuti ya mradi wa 'Kuwaleta ndani walio nje' ili kujifunza zaidi kuhusu wingi lugha darasani: multilingual-learning.com